# Vikwazo lukuki vinavyoathiri biashara

Inatoka Uk. 9

dokana na matatizo mengi yanayokwamisha uwekezaji likiwapo hilo.

Kimsingi Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) wakati wa uzinduzi huo limeelezea haja ya kuendelea kutengeneza mazingira bora ya biashara ili kufanya bidhaa zinazozalishwa nchini zikiwemo za huduma kushindana kimataifa.


Utafiti huo uliotoa taarifa ya hali halisi ya mazingira ya kibiashara kwenye nishati, uhafifu wa barabara, rushwa, upatikanaji wa maji usiokuwa na uhakika, fedha na kodi zinazopandiana unahitaji kufanyiwa kazi na hatua za makusudi kuchukuliwa kujitoa katika dhiki hiyo.

Ripoti pia imeonesha kuwa ipo haja kwa sekta za umma na sekta binafsi kushiriki katika kuwekeza kwenye uzalishaji wa umeme, maji, na miundombinu ya usafirishaji kwa sababu japokuwa kuna miradi inayoendelea, lakini bado safari ni ndefu, na kasi iliyopo ni ndogo.

Ni dhahiri utatuzi wa vikwazo vya biashara nchini kutasaidia wawekezaji wote wa ndani na watokao nje ya nchi kutengeneza bidhaa zenye ushindani na kuwezesha mabadiliko makubwa yanayohitajika katika uchumi wa Tanzania.

Alisema na kuongeza kuwa mitazamo ya viongozi wa biashara ambayo imetolewa kwa lengo mahsusi la kuchukua maoni ya jumuiya za biashara za Tanzania pia imeainisha ugumu uliopo wa kufanya biashara nchini.

Christine alisema ni matumaini yake kwamba changamoto zilizoelezwa katika ripoti hiyo zitafanyiwa kazi na kuisogeza Tanzania katika mazingira bora zaidi za ufanyaji biashara na uwekezaji.




**Katuni zinazokejeli uwekezaji.**

Katika masuala ya rushwa, ripoti imedokeza mambo yanavyokuwa kiasi cha kuwakatisha tamaa wawekezaji na pia kusaidia kuvunjwa kwa sheria na kusababisha matatizo kwa wawekezaji na hata walaji.

Kuna mambo mengi mno yanatolewa bure kwa watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa na kiulinzi na husababisha ukosefu wa haki za msingi kwa sababu inalinda wahalifu waliojificha.

"Siyo tu kwamba rushwa inawagharimu wafanyabiashara bali pia ni mchezo mchafu unaochezwa na kuwanufaisha wale wanaouhusika nao," alisema Kilindu wakati akizundua ripoti hiyo.

Kwenye ripoti, staili ya suala la rushwa imezungumzwa sana na hasa wafanyabiashara kutembelewa na wakaguzi kutoka mamlaka mbalimbali.

Ripoti inasema thamani za ukaguzi unaofanywa na mamlaka hizo ni mdogo kwa kuwa mara nyingi hatma ya ukaguzi huo ni kutishiwa kufungiwa biashara isipokuwa pale tu utakapoamua kulipa kitu kidogo.

Rushwa inapofua macho, lakini pia suala jingine ambalo limeonekana kuwa na shida ni upatikanaji wa mitaji hasa kuwepo kwa haja ya kuwa na dhamana bila kuwa na namna ya kusaidia kupatikana kwa dhamana kwa mikopo ya benki kwa watu katika sekta ya biashara.

Kumeelezwa na wengi wa waliohojiwa kwamba upatikanaji wa mitaji ni tatizo kutokana na kudaiwa dhamana ambayo wengi wa wajasiriamali hawana. Na matokeo yake viwanda vilivyopo vinashindwa kukua.

Pia miundombinu ya usafirishaji inasababisha kuwa na ughali wa kusafirisha mali ghafi na kusababisha bei nayo kutokuwa sawa.

Pia matatizo ya kodi kupandiana kumeelezwa kuwa shida na ripotri inashauri mabadiliko katika kodi ili kuwafanya wananchi wengi washiriki na hivyo kodi ilingane na thamani ya kitu na uwezo wa kushindana katika soko.

Ni dhahiri ripoti ya hali halisi ya mwaka jana kama itaangaliwa na Serikali inaweza kupata nafuu ya utafutaji wa majawabu ya kufanya bidhaa za Tanzania kuwa na ushindani.

SUDOKU 556